

Kupiga simu kwa 911



911 ni njia inayotambulika kitaifa, rahisi kukumbuka, isiokuwa na gharama yoyote ya kuwasiliana na watekeleza sheria, mashirika ya huduma ya moto na matibabu ya dharura. Kwa kuwa 911 ni ya hali za dharura, ni kawaida kushangaa kama kupiga simu ni jambo sahihi la kufanya. Hali za dharura ni hali yoyote ambayo mtekeleza sheria, wazima moto au msaada wa matibabu unahitajika. Ikiwa huna uhakika, piga simu kwa 911 na mchukua simu ataongea na wewe na kukupatia msaada unaofaa. Kupiga simu kwa 911 inafadhaisa, lakini wachukua simu wamefunzwa kukusaidia. Kujua unachopaswa kutarajia kunaweza kufanya kupiga simu kuwa rahisi na kupata msaada wowote unaohitaji.

Kupiga simu kwa 911

1. **KUWA MTULIVU!**

Ongea polepole na wazi.

2. **FAFANUA NI KWA NINI UNAPIGA SIMU...**

Fafanua ni nini unaripoti. Fafanua ikiwa hali ya dharura bado inaendelea au la. Wahudumu wa 911 watauliza maswali kuhusu Ni nani, Ni nini, Ni wapi, Lini, Kwa nini na Jinsi kuhusu hali ya dharura.

3. **SEMA ANWANI...**

Sema eneo/anwani halisi ya hali ya dharura. Jumuisha nambari za mtaa au ghorofa, sakafu, na maelezo yoyote ambayo yatasaidia wanaosaidia katika hali ya dharura kupata eneo sahihi.

4. **SEMA JINA LAKO NA ENEO LAKO LA SASA...**

Ijapokuwa haihitajiki, kusema jina lako husaidia na uchunguzi wowote unaofanyika.

5. **SEMA NAMBARI YA SIMU YA MAHALI UNAPOPIGIA SIMU...**

Sema maelezo haya iwapo maelezo zaidi yatahitajika baadaye.

6. **USITOKE KWENYE LAINI. USIKATE SIMU.**

Usikate simu hadi mhudumu wa 911 akate simu yako. Sema maelezo yote unayo. Hali hubadilika mara kwa mara na maelezo yaliyosasisiwa yanaweza kuhitajika.

SIMU ZA DHARURA:

- **Uhalifu unaoendelea**
- **Mkosaji katika eneo la uhalifu**
- **Mashahidi katika eneo la uhalifu**
- **Tukio lolote linalohusisha majeraha**

Kwa Hali za Dharura, Piga simu kwa 911

**T
I
P
S**

Kuwa MTULIVU!

Fafanua hali yako.

**Jibu maswali yote na ufuate maagizo
kama ilivyoagizwa.**

Idara ya Polisi ya Omaha
Kitengo cha Huduma za Mitaa
(402) 444-5772
OPDCrimePrevention@cityofomaha.org

WWW.OPD.CI.OMAHA.NE.US

505 South 15th Street
Omaha, NE 68102